

CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA NYANZA (1984) LTD.

Tel: +255 28 250 0299
E-mail: info@ncultd.or.tz

**NCU Building,
Kenyatta Road,
P. O. Box 9,
Mwanza.**

TANGAZO LA ZABUNI

Chama kikuu cha Ushirika Nyanza (1984) Ltd, kwa idhini iliyotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania kinawatangazia Wananchi, Makampuni, Taasisi mbalimbali kwamba kinauzi Vyuma chakavu.

Mahali vilipo Vyuma chakavu ni kama ifuatavyo:

A: Wilaya ya Nyamagana Jijini Mwanza

1. Igogo Rice mill-Mashine ya kukoboa mpunga (H- iron, U-iron na Angle iron zilizo beba mashine haviuzwi).
2. Kiwanda cha kukoboa Dengu Mrungushi Igogo -Mashine ya kukoboa Dengu.

B: Wilaya ya kwimba

1. Kiwanda cha Nyambiti Oil Mill -Mashine za kukamua mafuta
2. Kiwanda cha Mikokoteni Malya-Mashine za Karakana.

C: Wilaya ya Misungwi

1. Kiwanda cha Bukumbi-Mashine za kuchambua pamba.

D: Wilaya ya Sengerema

1. Kiwanda cha Nyamililo-Mashine za kuchambua pamba (H- iron, U-iron a Angle iron zilizo beba separator na cleaner haviuzwi).

E: Halmashauri ya Buchosa Wilaya ya Sengerema

1. Kiwanda cha Buchosa-Mashine za kuchambua pamba,
2. Kiwanda cha Buchosa oil mill -Mashine za kukamua mafuta.

F: Wilaya ya Ukerewe

1. Kiwanda cha Murutunguru-Mashine za kukamua mafuta,
2. Kiwanda cha Bugolora Rice mill -Mashine ya kukoboa mpunga.

NB: -Vifaa vya meme katika maeneo yote yaliyotajwa havitauzwa -Bahasha za zabuni zifungwe kwa rakili na kuandikwa juu "Zabuni ya Kununua vyuma chakavu Msimu 2024/25"

SIFA ZA MUOMBAJI .

- i. Awe na kampuni iliyosajiliwa kisheria (BRELA)
- ii. Awe na cheti cha usajili wa kampuni wa mamlaka mbalimbali za serikali.
- iii. Leseni halali ya biashara
- iv. Hati safi ya mlipa kodi (Tax clearance certificate)

-
- v. Awe na TIN namba
 - vi. VAT zinazotambuliwa kisheria
 - vii. Kibali cha kazi kutoka Mamlaka husika

MASHARTI.

1. Zabuni moja ya kununua Vyuma chakavu italipiwa ada isiyorudishwa (Non refundable) ya Tshs. 200,000/= Laki mbili tu fedha za kitanzania na zilipwe kwenye, ACCOUNT YA NMB; Namba 31110096999 JINA: NYANZA COOPERATIVE UNION (1984) LTD. Na pay-in slip iletwe Makao Makuu.
2. Wazabuni wote wanaruhusiwa kwenda kuona vyuma chakavu kwa gharama zao kabla ya kuomba zabuni. Wazabuni wote mnatakiwa kufika katika ofisi ya Meneja Mkoo wa Nyanza (1984) Ltd siku ya tarehe 18/03/2025 saa 3.00 asubuhi ili kupewa utaratibu wa kwenda kuona mali chakavu.
3. Mchakato wa zabuni utafanyika kwa njia shindani ya kitaifa (National competitive tendering) kwa mujibu wa mwongozo wa manunuzi na ugavi wa vyama vya ushirika Tanzania bara na sheria na kanuni za ununuzi wa zabuni ya wazi kwa wazabuni wote wenye sifa zinazohitajika
4. Mzabuni atakayetoa bei ya juu atalipa malipo ya awali (advance payment) asilimia ishirini na tano (25%) mara tu baada ya kumpata mshindi, atamalizia asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki ndani ya muda wa siku kumi na nne (14). Atakayeshindwa kumalizia asilimia (75%) iliyobaki baada ya siku 14, malipo ya wali hayatarudishwa na kifaa kitauzwa tena. Gharama zote za kuhamisha na kusafirisha kifaa kilichouzwa itakuwa juu ya mnunuzi.
5. Mnunuzi ataruhusiwa kuchukua kifaa baada ya malipo yote kukamilika.
6. Muda wa kutuma maombi ya zabuni ni siku kumi na nne tu (14). Kuanzia tarehe 15/03/2025 hadi tarehe 28/03/2025 saa 4:00 asubuhi. Na tarehe 28/03/2025 saa 5:00 asubuhi itakuwa siku ya ufunguzi wa zabuni. Wazabuni wote mnakaribishwa, eneo ni ukumbi mdogo wa chama kikuu Nyanza (1984) Ltd, zabuni zote zitapokelewa katika ofisi ya Meneja Mkoo kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

Zabuni zitakazochelewa kukusanywa hazitafanyiwa kazi wakati wa tathmini ya zabuni bila kujali sababu zozote za kuchelewa.

**Wananchi wote mnakaribishwa
Maombi yote yatumwe kwenda kwa:-
KAIMU MENEJA MKUU,
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA NYANZA (1984) LTD,
S.L.P 09, MWANZA.**